

## MAPAMBANO DHIDI YA BIDHAA BANDIA

Tume ya Ushindani (FCC) kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) and Jeshi la Polisi (dawati la hati miliki) tarehe 10 Aprili 2017 lilifanya ukaguzi kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa za mabati nchini katika mikoa ya Dar Es Salaam na Pwani.

Katika zoezi hilo Tume ya Ushindani ilifanikiwa kukamata mabati 108,923 yanayokadiriwa kuwa na thamani ya Sh. 2,175,000, 000 yanayodhaniwa kuwa ni bandia/ kutumika kutengeneza mabati bandia na malighafi zisizopungua 57 “Coils” zinazotumika kuzalisha mabati. Bidhaa tajwa zilikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 kama ilivyofanyiwa maboresho.

Baadhi ya bidhaa za mabati zilizokamatwa ni kama zinavyoonekana katika picha zifuatazo;



Mabati ya migongo mipana “IT Roofing Sheets” yaliyokamatwa.



Mabati ya rangi ya migongo midogo “Pre Coated corrugated Roofing Iron Sheets”



Mabati ya kawaida “GCI Roofing sheets”.



Mabati aina ya vigae “Profile versatile Roofing Sheets”.



Malighafi za kuzalishia mabati “Coils”.

### **TAHADHARI KWA UMMA**

Tume ya Ushindani (FCC) inautahadharisha umma wa watanzania kuhakikisha bidhaa za mabati wanazonunua zinamtambulisha mzalishaji na kuwa taarifa muhimu kwenye bidhaa hizo kwa namna ambayo haziwezi kufutika.

### **WITO KWA WAZALISHAJI, WASAMAMBAZAJI NA WAUZAJI WA REJA REJA BIDHAA ZA MABATI**

Tume ya Ushindani inawashauri kufuata sheria katika shughuli zao zote za kibiashara kwa kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa, kuingizwa kutoka nje zinamtambulisha mzalishaji halisi wa bidhaa husika na kuwa na taarifa muhimu zinazoitofautisha bidhaa yake na bidhaa nyingine zinazofanana au kushabihiana.